



## TAARIFA KWA UMMA

### TUZO ZA LATRA KWA WASAFIRISHAJI BORA NA SALAMA KWA MABASI YA MIKOANI NA NCHI JIRANI 2023/2024

*Dodoma, 09 Agosti, 2024*

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(a) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, pamoja na mambo mengine, Mamlaka ina wajibu wa kuhamasisha ushindani wenye ufanisi miongoni mwa watoa huduma zinazodhibitiwa. Katika kutekeleza sehemu ya wajibu huo, Mamlaka inaandaa tuzo za Wasafirishaji Bora na Salama kwa huduma za mabasi zilizotolewa kuanzia tarehe 01 Julai 2023 hadi 30 Juni 2024.

Tuzo hizo zitatolewa ili kuchochea matumizi ya mifumo ya utoaji wa huduma bora na salama ya usafirishaji wa abiria kwa ufanisi na ubunifu hususan katika matumizi ya teknolojia. Washindi watakabidhiwa Tuzo katika Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani yatakayofanyika tarehe 26 hadi 30 Agosti 2024 Mkoani Dodoma.

Washindani wamegawanywa katika makundi matatu; (i) Wasafirishaji **WAKUBWA** (wenye mabasi zaidi ya 30), (ii) Wasafirishaji wa **KATI** (wenye mabasi 11 hadi 30) na Wasafirishaji **WADOGO** (wenye mabasi matatu hadi 10).

Watumia huduma na wadau wote mnaombwa kushiriki kwa kuwapigia kura wasafirishaji kwa kuzingatia huduma zilizotolewa kwa kipindi husika. Vigezo na jinsi ya kupiga kura vinapatikana kupitia tovuti ya Mamlaka [www.latra.go.tz](http://www.latra.go.tz) kurasa za mitandao ya kijamii za LATRA au kiunganishi <https://forms.edodoso.gov.go.tz/x/Othf4u0Q>. **Mwisho wa kupiga kura ni tarehe 19 Agosti, 2024.** Kwa maelezo zaidi wasiliana na Mratibu wa mashindano kwa namba ya simu 0738 588 475.

Digitally Signed By Salum Pazy  
Fri Aug 09 03:56:19 EAT 2024

Salum Pazy

**MKUU WA KITENGO CHA UHUSIANO NA MAWASILIANO**



## VIGEZO VITAKAVYOTUMIKA KUMPATA MSHINDI

Wakati wa mashindano Vigezo na maeneo yatakavyotumika wakati wa mchujo na kumpata mshindi ni kama ifuatavyo:

### A. HUDUMA INAYOZINGATIA USALAMA (SAFETY)

Katika eneo hili, inatarajiwa kumpata msafirishaji mwenye:

1. Idadi ndogo ya matukio ya ajali yaliyotokea katika kipindi cha tathmini
2. Idadi ndogo ya ajali zilizosababisha vifo au majeruhi
3. Nyenzo/utaratibu wa Usimamizi/ufuatiliaji wa mabasi yakiwa safarini
4. Utaratibu wa kukatia mabasi bima inayostahili pamoja na ufuatiliaji wa fidia za abiria yanapotokea majanga
5. Mpango wa matengenezo ya magari unaotekelezwa
6. Mabasi yenye mikanda ya usalama kwenye viti iliyo safi na inayofanya kazi vizuri wakati wote
7. Madereva wanaoendesha kwa kuzingatia Sheria bila kuhatarisha maisha ya abiria na watumiaji wengine wa barabara

### B. HUDUMA YA UHAKIKA (SERVICE AVAILABILITY AND RELIABILITY)

Katika eneo hili, tunategemea kumpata msafirishaji mwenye;

1. Utaratibu wa Mabasi yake kufuata ratiba ya safari (muda wa kuanza safari, kupata huduma za kijamii)
2. Utaratibu wa kutoa taarifa muhimu za safari kwa wasafiri na wadau wengine (Ikiwepo kuwakumbusha abiria kufunga wa mikanda ya usalama, vituo vya kushuka na kupanda, huduma zinazopatikana ndani na nje ya basi,)
3. Utaratibu wa wasafiri kupata huduma anazozitoa kwa urahisi (ikiwepo ukataji wa tiketi kwa njia ya mtandao kwa mfumo uliunganishwa na Mifumo ya Serikali)

4. Utaratibu wa kutoza abiria viwango vya nauli vinavyotabirika visivyozidi viwango elekezi vilivyowekwa na Mamlaka
5. Matukio machache ya kusitisha safari kutokana na ubovu/uchakafu wa mabasi.

### **C. HUDUMA BORA KWA WATEJA (GOOD CUSTOMERM CARE)**

Katika eneo hili, inategemewa kumpata msafirishaji mwenye:

1. Urahisi wa kupatikana kwa huduma yake
2. Utaratibu wa kusikiliza na kushughulikia kero na Malalamiko yanayohusiana na huduma anayotoa
3. Utaratibu wa kusimamia na kutunza mizigo ya abiria kwa mujibu wa kanuni za usafirishaji
4. Utaratibu wa kutoa elimu kwa wateja (abiria na Umma)
5. Utaratibu wa kuzingatia vituo vya abiria kupanda, kushuka pamoja na kupata huduma za kijamii
6. Utaratibu wa kusimamia maudhui ya burudani zinazotolewa kwenye mabasi yake
7. Utaratibu wa kusimamia usafi na weledi wa wahudumu wa mabasi yake

### **D. UBUNIFU NA MATUMIZI YA TEKNOLOJIA (INNOVATION AND TECHNOLOGY)**

Katika eneo hili, inategemewa kumpata msafirishaji ambaye;

1. Anatumia nishati mbadala katika kupunguza uharibifu wa mazingira pamoja na gharama za utumiaji wa huduma
2. Ana ubunifu unaoweza kuwafanya wateja (abiria) kusafiri kwa raha zaidi
3. Anatoa huduma kwa abiria wenye mahitaji maalum ndani ya mabasi yake
4. Vifaa/vitu vinavyoweza kufanya safari kuwa ya furaha (Mfano vizuizi vya watoto kwenye basi (child restraints), WiFi, ving'amuzi, viburudisho nk)
5. Anatumia teknolojia ya habari kutoa taarifa kwa watumiaji wa huduma (mitandao ya kijamii nk)

6. Ana miundombinu ya kuhudumia abiria wenye mahitaji maalum ndani ya basi la mtoa huduma husika (miundombinu ya kupandia na kushuka kwenye mabasi kwa abiria wenye changamoto ya viungo, viti, mikanda ya usalama kwa abiria wote)

## **E. HUDUMA ENDELEVO (SUSTAINABILITY)**

Katika eneo hili, inatarajiwa kumpata na kumtambua msafirishaji ambaye:

1. Ametoa huduma ya usafirishaji kwa ufanisi kwa miaka mingi
2. Ana Mipango na mikakati bora na endelevu katika utoaji wa huduma ya usafirishaji
3. Anatoa ajira za uhakika na endelevu kwa jamii

Vigezo vingine vitakavyotumika katika kushindanisha watoa huduma ni pamoja na kuwapata wasafirishaji ambao wana:

- i. Tekeleza Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo na Masharti ya leseni za usafirishaji abiria nchini
- ii. Matukio machache ya makosa yanayohusu ukiukaji wa masharti ya leseni za usafirishaji
- iii. Matukio machache ya kusitishiwa leseni za usafirishaji
- iv. Matumizi sahihi ya Mfumo wa kufuatilia mwenendo wa Mabasi (VTS)
- v. Matumizi sahihi ya mfumo wa kutolea tiketi za kielektroniki (e-Ticketing)
- vi. Matumizi ya madereva wawili kwa mabasi yanayotoa huduma safari ndefu (safari za zaidi ya saa nane )
- vii. Wataalam wa usafirishaji/ biashara wa kusimamia mabasi yao
- viii. Wanatumia madereva waliosajiliwa na kuthibitishwa na Mamlaka
- ix. Wanatumia wahudumu waliopata mafunzo stahiki na kusajiliwa na Mamlaka.